

**KATIBU MKUU KIONGOZI AGAWA VITAMBULISHO VYA ZIADA VYA WAJASIRIAMALI WADOGO WA MKOA WA DAR ES SALAAM. 15-01-2019**

**1. UTANGULIZI**

Leo tarehe 15 Januari, 2019 Katibu Mkuu Kiongozi Balozi, Mhandisi John W. H. Kijazi aligawa **Vitambulisho 75,000** kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam Bw. Abubakar M. Kunenge. Huu ni muendelezo wa uzinduzi wa Vitambulisho hivyo uliofanywa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akifungua Mkutano wa Viongozi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa uliofanyika tarehe 10 Desemba, 2018 katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere - Dar es Salaam. Wakati wa uzinduzi huo, kila Mkuu wa Mkoa alipewa Vitambulisho Ishirini na tano elfu (25,000) kwa ajili ya kugawa kwa Wajasiriamali Wadogo.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na Bw. Andrew Massawe, Katibu Mkuu, Ofisi wa Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Ajira Vijana na Wenye Ulemavu; Mhandisi Joseph Nyamhanga, Katibu Mkuu TAMISEMI na Bw. Charles Kichere, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

**2. MWONGOZO WA UGAWAJI WA VITAMBULISHO**

Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania aliandaa Mwongozo wa kutambua wafanyabiashara wadogo na kugawa vitambulisho hivyo. Mwongozo huo uliwasilishwa kwa Wakuu wa Mikoa kupitia kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na hatimaye kwa Wakuu wa Mikoa. Vipengele vya Mwongozo huo ni:-

- 2.1. Mjasiriamali awe na Mauzo ghafi yasiyozidi Shilingi Milioni Nne (TShs.4,000,000/=) kwa mwaka.
- 2.2. Mjasiriamali awe hajawahi kusajiliwa na TRA na kupewa Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN) isipokuwa wale waliokwishaajiliwa awali na kupata kitambulisho au kama Mlipakodi.
- 2.3. Mjasiriamali anatakiwa ajaze fomu maalumu inayopatikana kwa Mkuu wa Mkoa kama mfanyabiashara wa Sekta isiyo rasmi (mfano. Mama/Baba Lishe, Mmachinga n.k) mfano wa fomu umeambatishwa.
- 2.4. Mjasiriamali atalipa Shilingi elfu ishirini (20,000/=) kwa Mkuu wa Mkoa. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa itaziweka pesa zote ilizokusanya kwenye akaunti ya Kamishna wa Kodi za Ndani kwenye benki zilizoidhinishwa

kukusanya Mapato. Fedha hizi zitalipwa kupitia mfumo wa malipo ujulikanao kama *Revenue Gateway System* (RGS) kupitia TIN ya Katibu Tawala wa Mkoa husika. Wakati wa usajili wa malipo kwenye RGS mlipaji atatumia *GFS code* 1111104. Baada ya malipo atapata risiti ya mtandao kwa malipo yote aliyowasilisha.

### 3. MUHTASARI WA UGAWAJI NA MAKUSANYO YA FEDHA

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli tarehe 10 Desemba, 2018 aligawa **Vitambulisho 650,000** vya Wajasiriamali wadogo kwa Wakuu wa Mikoa 26 ambapo kila mkoa ulipata vitambulisho 25,000. Aidha, Mkoa wa Dar es Salaam uliongezewa vitambulisho 25,000 na hivyo kufanya jumla ya vitambulisho vyote vilivyotolewa kwa mikoa yote 26 kuwa **675,000** hadi kufikia tarehe 13 Januari, 2019.

Hadi kufikia tarehe 13 Januari, 2019, jumla ya **Vitambulisho 104,773** vilikuwa vimeshagawiwa kwa Wajasiriamali wadogo katika mikoa yote 26 na jumla ya **Shilingi 2,095,460,000.00** zilikuwa zimekusanywa.

**Vitambulisho 75,000** alivyogawa Katibu Mkuu Kiongozi kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam leo tarehe 15 Januari, 2019 vinafanya Mkoa wa Dar es Salaam kuwa na **Vitambulisho 125,000**.

### 4. MAELEKEZO YA KATIBU MKUU KIONGOZI

Katibu Mkuu Kiongozi alielekeza kuwa:

- 4.1. Wakuu wa Mikoa wawe wanatoa taarifa ya vitambulisho vilivyotolewa kwa Wajasiriamali wadogo pamoja na fedha zilizokusanywa kila wiki,
- 4.2. Fedha zote ziwe zinawekwa kwenye akaunti ya TRA kila siku na Katibu Mkuu TAMISEMI awe anafuatilia taarifa za kugawa vitambulisho na uwasilishaji wa fedha kwenye akaunti ya TRA,
- 4.3. Kusiwe na mianya ya watu kujipatia fedha kupitia zoezi la kugawa vitambulisho hivyo kwa kuuza kwa bei zaidi ya Shilingi 20,000,
- 4.4. TRA wahakikishwe kuwa zoezi hili halitasababisha kupoteza walipa kodi walipo sasa.